## Carta de Rehema Muhatobe

Nací el 20 de abril del 2004 en Mahenge en la provincia de Iringa. Somos cuatro hermanos yo soy la segunda. Vivo con mi madre a mi padre no le conozco. Mi madre cultiva el campo pero nuestra vida no es buena. Cuando terminé la primaria la escuela a la que podía ir estaba muy lejos, iba andando y si llegaba tarde me castigaban. Eramos muchísimos alumnos y no había sillas ni mesas para todos, tuve que dejarlo era imposible continuar Pero mi madre no podía pagar un colegio para mi es muy pobre. Por medio de una persona que conocía Educa me dieron la oportunidad de estudiar en el Colegio Educa Secondary, y cambió mi vida, estoy muy contenta.

Aquí disponemos de todo lo necesario como comida, cama y la ropa, las cosas de aseo, los libros…y nuestros profesores nos enseñan son buenos. Soy feliz. Agradezco a la gente de Educa porque me salvasteis. Os pido no perdáis vuestro buen corazón.

Gracias

HISTORIA YA MAISHA YANGU. Rehema - Mwakatobe. 24-10-2018

Jina langu ninaitwa Rehema Mwakatobe. Nimezaliwa tarehe 20/04/2005 katika kijiji cha cha Mahenge wilaya ya kilolo, mkoa wa Iringa. katika familia yetu tupo wanne 4. Wa kwanza ni dada yangu, wapili ni mimi na watatu na wanne ni Wadogo zangu. Ninaishi na mama yangu tu. kwa sababu baba yangu simjui. Mama yangu ni mkulima pia ni mfanyabiashara ndogo ndogo. pia maisha yetu nyumbani sio mazuri ni ya kawaida tu. Nimeanza shule mwaka 2011 na nimemaliza darasa la saba mwaka 2017. Na nilifanikisha kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Lukosi. Nilipofika shule ile haina madarasa ya kutosha na pia haina viti na meza za kutosha Nilikuwa nasoma kwa taabu Inakubidi uwahi shuleni na Usafiri ni wa tabu. na ukichelewa kufika shule unapigwa na adhabu unapewa. tulikuwa tunakaa kwa kubanana na viti vilikuwa Vichache. kwa hiyo nilikuwa nasoma hivyo hivyo na Jumla ya kidato cha kwanza tulikuwa 410 na shule nzima tulikuwa 856. Ilikuwa tarehe 22-03-2018 ambayo ilikuwa Alhamisi nilikuja shule hii nzuri ya educa. shule hii nimeipenda kwa sababu ina mazingira mazuri ya kujisomea na haina Vishawishi Vitavyoweza kusababisha wanafunzi kuacha shule. Ninaamini mungu atanisaidia nitafanikisha ndoto zangu za kuwa Nesi au Mwandishi wa habari. Ninasoma ili niweze kumsaidia mama yangu huko nyumbani kwa sababu mama ananitegemea sana nitaweza kumsaidia baadaye. Na pia shule hii nimeipenda kwa sababu inavitu muhimu vya kimasomo kwa mfano Chakula, malazi na nguo za shule pia. Naipenda sana kwa sababu nikikumbuka hali ya shule ya sekondari Lukosi ni tofauti kwasababu Inaviti vya kutosha, meza na mabafu navyoo vya kisasa.

Shukrani kwako sana Mama pilar kwa kunisaidia mimi Rehema kuja hapa shuleni ili nisome nije kuokoa maisha yangu na wazazi wangu na ndugu zangu Lakini kukufurahisha ili uwe na matumaini ili kujitolea moyo huohuo. Nakushukuru sana kwa wema wako ulionite ndea. Endelea kuwa na moyo mmoja wa kusaidia watoto kama sisi

Asante